**KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**(MASIJALA KUU)**

**DAR ES SALAAM**

**MAOMBI MADOGO NA. 34 YA MWAKA 2022**

**MWL. EZEKIAH TOM OLUOCH......................MLALAMIKAJI**

**DHIDI YA**

**KATIBU MKUUU KIONGOZI...................MLALAMIKIWA WA KWANZA**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI......MLALAMIKIWA WA PILI**

**UAMUZI**

9/9/2022 & 30/9/2022

**MZUNA, J.:**

Maombi haya yameletwa kwa mujibu wa kifungu cha 2(1) na 2(3) cha Sheria ya Matumizi ya Sheria "The Judicature and Application of Laws Act" Sura ya 358, Toleo la 2019 na kifungu cha 17 (2) cha Sheria ya "the Law Reform (Fatal Accidents and Miscellaneous Provisions) Act", Sura ya 310 Toleo la 2019, Kanuni ya 8(1) (a),(b na 8(2) ya Law reform (Fatal Accident and Miscellaneous Provision) (Judicial Review Procedure and fees) Rules ya mwaka 2014 Tangazo la Serikali Na. 324 la mwaka 2014 na Kifungu cha 95 cha Sheria ya Mwenendo wa Madai [Sura ya 33 Marejeo ya mwaka 2019].

Mwombaji ameomba pamoja na mambo mengine itolewe Amri ya "*certiorari*" *ya* kufuta na kuweka kando barua ya Katibu Mkuu kiongozi ya terehe 6/1/2022 yenye kumb. Na. CAB.30/536/PF.636/15 iliyomjulisha mleta maombi kwamba rufaa aliyokata kwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania imetupiliwa mbali, kwamba mahakama hii itamke kuwa maamuzi ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kama mamlaka ya rufaa ni batili, mahakama itoe gharama za shauri hili kwa Mleta maombi pamoja na nafuu zingine itakayoona zinafaa kutolewa kwa muombaji.

Pamoja na maombi hayo ya msingi, muombaji aliomba taarifa itolewe kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa anapaswa kuwasilisha nyaraka mbalimbali muhimu katika Mahakama hii kwa kuwa zinahusiana na kesi iliyofunguliwa.

Mleta Maombi baada ya kuleta maombi hayo hapa mahakamani upande wa wajibu maombi waliwasilisha pingamizi moja la awali la kisheria kwamba:-

1. ***Maombi haya yamekinzana na kanuni ya 8 (1) ya the law reform (Fatal Accidents and Miscellaneous Provisions) Judicial Review Procedure and Fees) Rules, 2014.***

Wadaawa wa pande zote mbili walikubalina kwamba pingamizi hilo la awali lisikilizwe kwa njia ya maandishi. Waleta Pingamizi waliwakilishwa na Wakili wa Serikali Bw. Daniel Nyakiha, na Mjibu Pingamizi alijiwakilisha mwenyewe.

Bwana Nyakiha aliwasilisha kuwa maombi yaliyotumika kuomba ruhusa mbele ya Mahakama hii siyo hayo yaliyowasilishwa wakati wa kuomba ruhusa ya kusajili shauri hili, yaani Mleta Maombi ameongeza baadhi ya maelezo ambayo hayakuwepo wakati akiomba ruhusa. Mleta Pingamizi aliendelea kusema kuwa katika ombi lililowasilishwa na Mleta Maombi, tarehe 04 mwezi Mei 2022 kwenye kiapo chake aliandika aya **57** tu, kuanzia ukurasa wa 5 hadi 22.

Baada ya mahakama kukubali ombi la ruhusa, Mleta Maombi alifungua maombi haya ya msingi, tarehe 20 mwezi Agosti 2022, aliandika aya **81** kuanzia ukurasa wa 14 hadi 41. Aidha, katika maelezo ya Mleta Maombi (statement) kulikuwa na mabadiliko tofauti na Maelezo yaliyotumika katika kuomba ruhusa, ikiwa ni kinyume na kanuni ya **8 (1) ya 'the law reform (Fatal Accidents and Miscellaneous, Provisions) Judicial Review Procedure and Fees) Rules, 2014.** Bwana Nyakiha alifafanua kuwa kwa mujibu wa kanuni tajwa ni wazi kuwa alichokiomba kwenye ombi la ruhusa

(leave) ndicho kilichopaswa kuandikwa kwenye kesi ya msingi bila mapungufu au nyongeza ya aina yoyote. Maneno yaliyotumika ni *"in respect of which leave was granted"*.

Sambamba na hilo, katika shauri la kesi ya msingi Mleta Maombi ameandika vitu vingi vya nyongeza ambavyo awali alivyoomba ruhusa ya mahakama havikuwepo. Aliongeza kwa kusema kwenye kesi ya msingi ni lazima aombe ruhusa ya mahakama kama ilivyotajwa katika sheria za madai, Amri ya VI Kanuni ya 17 ya Mwenendo wa mashauri ya Madai, [Sura ya 33 Marejeo ya 2019]. Kitendo cha muombaji kutoomba ruhusa ya mahakama na kujiamulia mwenyewe kuongeza aya 24 kwenye kesi ya msingi ambazo mwanzo hazikuwepo katika ombi la ruhusa ambayo mahakama ilitoa ridhaa kwa muombaji kufungua shauri la msingi ni kinyume na matakwa ya sheria.

Ili kuweka msisitizo Bwana Nyakiha amerejea kesi iliyoamuliwa na Mahakama ya Rufani katika kesi ya **George M. Shambwe v. Attorney General and Another** [1996] TLR 334 (CAT), kuwa mahakama itaruhusu marekebisho ya majibizano ya nyaraka za mashtaka ikiwa imejiridhisha na matakwa matatu; Kwanza maombi yameombwa kabla haijaanza kusikilizwa; Pili, marekebisho hayo yana umuhimu sana katika kuleta haki kwenye pande zote mbili; Tatu, hayo marekebisho yasivunje haki. Hivyo alisisitiza kuwa

kitendo cha mleta maombi kufanya marekebisho bila ruhusa ya mahakama ni kinyume na kanuni ya 8(1) ya 'the Law Reform (Fatal Accidents and Miscellaneous Provisions) Judicial Review Process and Fees) Rules, 2014.'

Kitendo hicho kinawanyima upande wa pili hoja za kubishaniwa au kutoa mwanya kwa Mahakama kuamua kuwa kuna shauri la msingi au hakuna. Pia ni uthibitisho kuwa Mleta Maombi alikuwa na nia ovu ya kupata ruhusa ya Mahakama kwa kuficha baadhi ya maelezo. Alihitimisha kwa kuwasilisha kuwa ni rai ya Waleta Pingamizi Mahakama hii itupilie mbali maombi haya.

Mleta maombi alijibu pingamizi kwa kuibua hoja moja kwamba pingamizi lililoletwa na Wajibu maombi halikidhi kuwa pingamizi kwa kuwa halina msingi wa sheria. Alifafanunua kuwa ili pingamizi hilo liweze kuamuliwa na mahakama hii tukufu ni lazima mahakama hii ikatafute ushahidi dhidi ya mawasilisho yaliyoletwa na wajibu maombi ili kujiridhisha kama kweli kuna aya ambazo zitakuwa zimeongezwa na Muombaji katika maombi yake ya mapitio ya kimahakama *Judicial Review* baada ya kupewa ruhusa. Kwamba Mahakama italazimika kufanya utafiti Kwa kuitisha Jalada la Kesi ya ruhusa (leave) lililokwishafungwa na Mahakama hii kwenye Misc.

Civil Application No.10 ya mwaka 2022 ambayo Muombaji alileta mbele ya Mahakama hii na kufanyiwa maamuzi na Mahakama.

Mleta maombi alitetea hoja yake kwa kurejea katika maamuzi mbalimbali ya mahakama za juu yanayosema kuwa sio kila pingamizi ni pingamizi lenye msingi wa sheria na pingamizi lolote linaloibua hoja ya ushahidi ili liweze kuamuliwa, halikidhi kabisa kuwa pingamizi lenye mashiko ya sheria kama ilivyoamuliwa kwenye kesi ya **Mukisa Biscuit Co. Vs West End Distributors** (1969) EA 696.

Aliijulisha Mahakama maamuzi katika kesi ya **Shose Sinare Vs Stanbic Bank Tanzania Ltd and Another** (unreported) akisema haipaswi kutumia vielelezo kushughulikia pingamizi la awali. Alisisitiza kuwa si kweli kuwa Mahakama hii haijafungwa mikono kupitia maelezo yaliyomo katika maombi ya ruhusa bila kuvunja sheria bali ukweli ni kwamba Mahakama itakaposhawishika na kufanyia kazi maombi ya wajibu maombi na kupitia nyaraka za shauri la ruhusa ili kutafuta tofauti hizo itakuwa imevunja msingi ulioainishwa katika kesi ya **Mukisa Biscuits Co.** (Supra).

Mleta Maombi aliongeza kuwa Amri ya VI Rule 17 ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33 (Marejeo ya 2019) haitumiki katika mazingira

ya shauri hili kwa sababu shauri hili Namba 34/2022 ni shauri jipya na halijafanyiwa marekebisho na hoja yao imejikita kana kwamba Shauri Na. 34 ya mwaka 2022 lilifanyiwa marekebisho na Mwombaji. Na kesi ya **George M. Shambwe Vs Attorney General and Another** (Supra) haiwezi kutumika katika shauri hili kwani mazingira yake ni tofauti.

Aidha Mleta maombi aliwasilisha pia kwamba, endapo Mahakama hii tukufu itaona kwamba pingamizi la wajibu maombi lina mashiko, nafuu ya muombaji ni kuondoa au kutozingatia aya ambazo walalamikaji wameona kwamba zimeongezwa katika maombi ya muombaji kwa kurejea kesi za **S. Mkumba na mwenzake Vs. Attorney General,** Civil Application No. 240/01 of 2019 (Unreported) iliyonukuu kesi ya **Chadha & Company Advocates v. Arunaben Chaggan Chhita Mistry & 2 Others,** Civil Application No. 25 of 2013 ambapo mahakama ilisema kwamba;

> *"Where the offensive paragraphs are inconsequential, they can be expunged leaving the substantive parts of the affidavit remaining intact so that the court can proceed to act on it."*

Kwa kuhitimisha mleta maombi aliomba pingamizi liweze kuondolewa (dismiss), na kama mahakama hii itaona pingamizi lililoletwa na Wajibu maombi linamashiko, kwa kupitia kifungu cha 3A,3B na 95 cha Sheria ya

Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33, (Marejeo ya 2019) na Ibara ya 107A (1) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania iliyorejewa mara kwa mara, aya ambazo zinalalamikiwa na wajibu maombi ziweze kuondolewa au kutozingatiwa na Mahakama ili Mahakama iendelee na shauri ili muombaji aweze kupata haki yake ya msingi ya kikatiba ya kusikilizwa.

Wakili wa wajibu maombi alitoa maelezo ya nyongeza "rejoinder" kuwa mawasilisho ya Mleta Maombi hayajajibu pingamizi la kisheria lililowasilishwa mbele ya Mahakama. Kwamba Mleta Maombi kwenye mawasilisho yake ni kama amekubali kuwa nyaraka zake zilizotumika kwenye maombi ya ruhusa ni tofauti na nyaraka alizowasilisha katika shauri la msingi kwa kuomba Mahakama iondoe aya ambazo zimeongezeka. Hali hii ni kama kukubali kuwa kuna aya zimeongezeka na kwa hali hiyo ni wazi kuwa maombi yaliyotumika kwenye maombi ya kibali "leave" sio hayo yaliyotumika kwenye maombi ya msingi. Kwamba Mleta Maombi alikusudia kuipotosha Mahakama kwa kutumia maombi tofauti na yale yaliyompa ruhusa.

Na kwa kurejea kifungu cha 8 (1) Kama maombi yaliyotelewa ruhusa yanapoonekana sio yale yaliyowasilishwa Mahakamani basi Mahakama hii ina mamlaka ya kutamka kuwa maombi haya ni batili na kuyaweka kando.

Alipinga maelezo kuwa pingamizi lililowekwa halikidhi matakwa ya shauri la **Mukisa Biscuits Co. vs. West End Distributors** (Supra).

Aliongeza kuwa matakwa ya sheria kwamba unapochambua pingamizi la awali unatakiwa kuzingatia kilichomo kwenye nyaraza za kimahakama za wadawa (pleadings) pamoja na viambatishi vyake. Hali hii ya kisheria imewekwa wazi na Mahakama ya Rufaa, katika shauri la **Moto Matiko Mabanga vs Ophir Energy Plc and 6 Others,** Civil Appeal No. 119 of 2021. Alisisitiza kuwa kwa mujibu wa pingamizi, Maombi haya yanapingana na Kanuni ya 8 (1) (a) ya sheria, hivyo ni rai yake mahakama hii iyafukuze (struck out) maombi haya ya mleta maombi kwa kuwa yapo kinyume na kanuni na sheria.

Baada ya kusikiliza kwa kina na kupitia kwa makini mawasilisho ya pande zote mbili, *nitajielekeza katika kutambua endapo pingamizi la awali lililoletwa lina sifa za pingamizi ya awali kama zilivyoainishwa katika kesi ya **Mukisa Biscuit** au la?*

Hoja hii ni muhimu ili Mahakama iweze kujielekeza vizuri katika misingi iliyokwisha wekwa ya sifa za Pingamizi linalotakiwa kusikilizwa katika hatua za awali. Kwa mujibu wa kesi ya **Mukisa Biscuit** (Supra) pingamizi la awali

ni lile lililojikita katika hoja za kisheria ambazo hazihitaji Ushahidi kuthibisha, kama mamlaka ya Mahakama na shauri kupitwa na muda. Mahakama ilisema hivi:-

> *"...**a preliminary objection consists of a point of law which has been pleaded, or which arises by clear implication out of pleadings,** and which if argued as a preliminary point may dispose of the suit. Examples are an objection to the jurisdiction of the court or plea of limitation, or submission that the parties are bound by the contract giving rise to the suit to refer the dispute to arbitration."*

Msisitizo ni wangu.

Katika shauri hili pingamizi la awali limejikita kwamba maombi ya msingi ya mleta maombi alikiuka kanuni ya 8 (1) ya 'the Law Reform (Fatal Accidents and Miscellaneous, Provisions) Judicial Review Procedure and Fees) Rules, 2014. Kanuni ya 8(1) inasomeka hivi;

> *"Where a leave to apply for judicial review has been granted, the application shall be made-*
>
> *(a) by way of chamber summons supported by **an affidavit and statement in respect of which leave was granted."***

Kwa mujibu wa maelezo ya wajibu maombi, mleta maombi alikiuka kifungu hicho kwa kuongeza aya katika kiapo cha maombi ya shauri la msingi na pia kwa kuongeza taarifa zaidi katika kiapo ambazo hazikuwepo katika

kiapo cha shauri la maombi ya ruhusa. Aya zinazolalamikiwa katika kiapo pia zilizokiuka kanuni ya 8(1) ni aya ya 15, 16 na 25, 27, 28, 31, 32, 33, 35, 36, 38, 39 40, 41, 42, 46, 47 na 48 za kiapo cha mleta maombi.

Kwa maelezo ya mleta maombi mwenyewe amekiri kutenda kasoro hiyo ambayo ni kinyume na takwa la sheria. Dai la kwamba ili Mahakama iweze kujiridhisha kwamba aya tajwa zina makosa au la, Mahakama inahitaji ushahidi kwa kupitia kiapo cha mleta maombi kilichokuwa kimeambatanishwa katika shauri la maombi ya ruhusa ambacho hata hivyo hakikuambatanishwa katika shauri hili la msingi hazina mashiko. Nasema hivyo na kukubaliana na maelezo ya wakili wa wajibu maombi kwamba pingamizi la awali laweza kuthibitishwa pia kwa kuzingatia maneno (pleadings) kama ilivyoainishwa katika kesi ya **Moto Matiko Mabanga vs Ophir Energy Plc and 6 Others** (Supra) ambayo katika ukurasa wa 14, Mahakama ya Rufaa ikirejea shauri la **Ali Shabani and 48 Others v. Tanzania National Roads Agency and The Attorney General,** Civil Appeal No. 261 of 2020, ilisema kuwa;

> *"It is clear that an objection as it were on account of time bar is one of the preliminary objections which Courts have held to be based on pure point of law whose determination does not require ascertainment of facts or evidence. At any rate, we hold the view that no preliminary objection will*

*be taken from abstract without reference to some* ***facts plain on the pleadings which must be looked at without reference examination of any other evidence."***

Maamuzi hayo hapo juu Mahakama ya Rufaa ilieleza bayana kuwa Mahakama hii haijafungwa kuangalia baadhi ya maelezo katika "pleadings" ili kufikia maamuzi sahihi, (nionngeze, hasa pale ambapo sheria husika imesema bayana).

Niseme pia kwamba nimepitia maamuzi katika shauri la **Shose Sinare Vs Stanbic Bank Tanzania Ltd and Another,** (supra) ambapo Mahakama ya Rufaa ilinukuu maamuzi ya awali ya kesi ya **Soitsambu Village Council, Vs. Tanzania Breweries Ltd and Another,** Civil Appeal No. 105 of 2011 (unreported) ambapo iliamua pamoja na mambo mengine kwamba: -

> *"The court must therefore insist on the adoption of the proper procedure for entertaining applications for preliminary objections. It will treat as a preliminary objection only those points that are pure law, unstained by facts or evidence..."*

Siyo kwamba *"court needs to investigate such facts..."* Jambo hili ndiyo hasa ninalolifanya sasa siyo kuangalia jambo linalobishaniwa linalohitaji ushahidi. Mfano suala la "leave" halina ubishi na ndiyo hasa "pleaded facts in the affidavit and statement" siyo kuleta mambo mapya na

kujenga kesi upya. Mfano pingamizi limeeleza kwa mujibu wa maelezo ya Mjibu Maombi kuwa Mleta Maombi ameandika vitu vingi vya nyongeza ambavyo awali alivyoomba ruhusa ya mahakama havikuwepo, kama ifuatavyo;

(i) *Katika kesi ya msingi kwenye kiapo cha muombaji, ukurasa wa 17, aya ya 15, muombaji ameongeza taarifa ambazo hazikuwepo katika aya ya 15 kwenye ombi la mahakama ambalo mahakama imempa ruhusa. Muombaji ameongeza maneno yafuatayo '...na katika kipindi chote cha likizo bila malipo tarehe 27 Mei mwaka 2015 mlalamikaji alijulikana na kutambulika kuwa alikuwa mtumishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na si mwajiriwa wa Manispaa ya Ilala.'*

(ii) *Pia aya ya 16 katika ombi la ruhusa ambayo mahakama ilitoa ridhaa, ni tofauti na aya ya 16 kwenye kesi ya msingi.*

(iii) *Kwamba kwenye kesi ya msingi, aya ya 25, 27, 28, 31, 32, 33, 35, 36, 38, 39 40, 41, 42, 46, 47, 48 haikuwepo kwenye ombi la ruhusa ambayo mahakama ilitoa ridhaa.*

(iv) *Aya ya 26, 27 na 28 katika ombi la ruhusa ambayo mahakama ilitoa ridhaa, haipo kwenye kesi ya msingi.*

(v) *Katika maelezo ya mleta maombi (statement) maombi yaliyopo katika aya 4 (b) ni tofauti kabisa na yale yaliyokuwepo katika maombi ya ruhusa. Ambapo katika aya 4(b) imeongeza vipengele (i-xviii) ambavyo mleta maombi hakuweka wakati anaomba kibali cha kufungua mapitio ya mahakama.*

Hayo yote ni mapya hivyo pingamizi linakidhi vigezo na ninalikubali.

*Kama hivyo ndivyo, nini sasa kifanyike kwa kuzingatia matakwa ya sheria kuwa mahakama zijikite zaidi katika kutenda haki na siyo kujali zaidi mambo ya kiufundi?*

Nianze kwa kusema kuwa si kweli kwamba kiapo kilichotumika katika maombi ya ruhusa hakiwezi kurekebishwa. Kwa kuwa kiapo hicho kiliweza kuishawishi Mahakama kwamba mleta maombi ya ruhusa alikidhi vigezo vyote vya kupewa ruhusa (leave), hivyo maudhui hayohayo pia yanapaswa kutumika katika shauri la Msingi baada ya kuruhusiwa. Kinachopaswa kubadilishwa ni lengo/nafuu zinazoombwa sasa.

Kwa kuwa pingamizi hili limekidhi vigezo vya kisheria, Mahakama hii kwa kuzingatia maamuzi ya Mahakama ya Rufani katika kesi ya **Jamal S. Mkumba & Another v. Attorney General** (Supra) inampa nafuu mleta maombi arekebishe maombi yake ya maelezo na kiapo (to file supplementary or amended statement and affidavit) ili vijikite zaidi katika aya zilizotumika kuomba kibali "leave".

Ninasema hivyo kwa sababu katika kesi hiyo ya **Jamal S. Mkumba & Another v. Attorney General**, (Supra) kulikuwa na pingamizi juu ya uthibitisho wa kiapo "verification" ambapo hoja ililetwa kuwa kinapaswa

kutupiliwa mbali kwa sababu hakuonesha kati ya aya zake zipi alikuwa anazijua mwenyewe na zipi ni aya za kuambiwa. Mahakama ya Rufani ilihukumu kuwa:-

1. *Kila kesi inaamuliwa kulingana na mazingiya yake "each case has to be decided depending 'on its own merits'"*
2. *Pia kuzingatia haki ya msingi "regard to '**substantive justice**'".*
3. *Na kwamba mjibu maombi hatapata madhara yoyote iwapo marekebisho yatafanyika katika maombi hayo **"the respondent will not be prejudiced by an order of amendment of the affidavit so as to accord a chance to the applicant to insert a proper verification clause according to law and parties be heard on merits."***

(Msisitizo ni wangu).

Baada ya kusema hayo mahakama iliruhusu kufanyika marekebisho "Amended affidavit".

Hivyo pingamizi nalikubali ila maombi hayatafutwa bali mwombaji anaruhusiwa kufanya marekebisho hayo kwa kuleta kiapo kipya na maelezo mapya, siyo kuondoa "expunge" yale yaliyozidi tu au kuendelea na kiapo kile kile kama alivyoomba. Hii inatokana na ukweli kwamba aya alizoziongeza ni nyingi sana tofauti na ilivyokuwa katika kesi ya **Anna Makanga v. Grace**

**Woiso,** Civil Reference No. 2/2006 (Unreported) aliyoisema mleta maombi ambapo ni aya moja tu ya saba (7) iliyokuwa 'expunged'.

Hivyo Mleta maombi afanye marekebisho hayo ndani ya muda wa siku saba tokea leo tarehe ya uamuzi. Kila Mdawa "Party" abebe gharama zake. Imeamuliwa hivyo.

HIGH COURT OF TANZANIA

**M. G. MZUNA,**

**JAJI.**

**30 SEPTEMBA, 2022.**

*Imesainiwa hapa Dar es Salaam leo tarehe 30 ya mwezi Septemba, 2022.*